# Je, Petro Alikuwa Papa Wa Kwanza?

Hakika hatuna chuki kuhusu Wakatoliki. Tunapenda kuwasaidia ili waone na kufanhamu ukweli unaowafany watu kuwa huru.

Tunakaribisha kujifunza kwa waangalifu kuhusu swali hili. Mengi yanaegemeo lao juu ya jibu lililosahi hi. Hakuna mwisho unaoweza kufikiwa uliohakika zaidi kuliko msingi unaposimama. Basi, tuwe waangalifu kwamba imani yetu isisimamia juu ya chanzo kilicho fikiriwa cha mashaka, na kisicho thibitishwa. (Tazama, Maandiko yote ni kutokana na tafsiri ya Kikatoliki, Nakala za chama, Imprimatur, Francis Kardinali Spellman).

Kama mwisho haauwezi kufikiwa kuwa Petro alikuwa Papa wa kwanza, kama wanavyodai rafiki zetu wa Kikatoliki, kwa hiyo, inafuata, kwamba wanajenga ju ya dhana tu, au neno lisilohakikishwa.

Kama linawezakuhakikishwa kuwa Petro hakuwa Papa wa kwanza, jiwe la pembeni la Katoliki litaondolewa, msingi utabomoka, na jingo nzima kuanguka.

Kabla hawajachukuwa nafasi yao Wakatoliki lazima wathibiishe:

1. Kwamba Kristo alitaka mtu Fulani kuwa kichwa cha kanisa hapa ulimwenguni na kushikilia nafasi ambayo Papa anashikilia.
2. Kwamba warithi watakuwa wanateuliwa kushika nafasi hiyo.
3. Kwamba Petro alichaguliwa kushika nafasi hiyo.
4. Kwamba Petro alikuwa na anatumia mamlaka yake juu ya mitume wengine na kanisa nzima.
5. Pia, lazima wahakikishe kuwa mamlaka hiyo ilihamishiwa kwa wengine, na:
6. Kwamba nguvu za ishara za Petro zilihamishiwa kwa wengine katika vizazi kwa sababu mamlaka ya cheo cha Mitume ilihifadhiwa na kuimarishwa kwa nguvu za ishara.

## Kutumia Vibaya-Dhana Tu

Kutokana na Luka 22:31, 32 ambapo Yesu alimwambia Petro kuwa anamwombea, na "utakapoongoka waimarishe ndugu zako," Wakatoliki hujifanya kwamba Yesu alikuwa akimpa Petro nguvu za Papa juu ya Kanisa. Lakini mstari nausemi hivyo wala haufunidishi hivyo. (1) Yaonekana kwamba Yesu alifahamu udhaifu wa Petro, ya kwamba atamkana. (2) Paulo na sila "walipita katikati ya Siria na Kilikia, na kuyaimarisha makanisa" (Mdo. 15:41). Je hili laonyehsa kwamba Paulo na Sila walikuwa Ma-Papa? (3) Hata kidogo, mstari haujaanza kuonyesha kwamba Yesu alimfanya Petro kuwa Papa.

Kutoka katika Yohana 21, ambapo Yesu alimwambia Petro "kulisha kondoo zake," Wakatoliki husema kuwa Yesu alimfanya Petro kuwa kichwa cha kanisa na Papa. Hata hivyo jawabu la aina hiyo ni wazo tu. Hakuna mafundisho kama hayo katika mstari.

Yesu alipomwuliza Petro kama alimpenda kuliko “hawa,” hakuwa na maana ya “hawa” mitume wengine. (1) Petro hakuweza kufahamu wenzie walimpenda kiashi gain; (2) Kwa Petro kuhakikisha kwamba alimpenda Yesu kuliko Mitume wengine walivoympenda kungeamsha majadiliano na faraka kati yao. Yesu aliomwambia Petro “lisha kondoo wangu” hakumfanya kwa namna yeyote kuwa Papa. Wakatoliki wasemapo kwamba Yesu alikuwa na maana ya watu, ni dhana tu. Paulo aliwaamuru waze pale Efeso “kulisha kanisa la Bwana” (kulitawala kanisa la Mungu) (Tafsiri ya Kikatoliki) Je, kuliwafanya wazee hao kuwa Ma-Papa? Hasha.

I. Umashuhuri Hauthibitishi Kazi Wala Heshima

Wakatoliki hubisha kwamba kwa sababu ya umashuhuri wake Petro lazima alikuwa Papa na mwenye mamlaka juu ya mitume wengine. Kwambab jina lake mara nyingi limetajwa kwanza, na kwamba alikuwa mashuhuri kati ya Mitume – halikataliwi. Hata hivyo mambo haya hayathibitishi kwamba alikuwa na mamlaka juu yaw engine, au kwamba alikuwa na cheo kile cha Papa wa siku hizi.

Angalia mambo haya:

a. Jina lake halikuwa la kwanza kila mara. Andrea aliitwa kwanza. Kisha alimpata Petro na kumleta kwa Yesu, Yoh. 1:14.
b. Kama jina la Petro lilitajwa kwanza kila siku, hili halithibitishi kwamba alikuwa kwanza katika cheo au mamlaka.
c. Yakobo, sio Petro, alikuwa mashuhuri katika mkutano wa Yerusalemu, Mdo. 15:14-21.
d. Yakobo, sio Petro, ametajwa kwanza katika Wagalatia 2:9.
e. Mwishoe, kama Petro alikuwa ametajwa kwanza katika kila nafasi halithibitishi kwamba alikuwa Papa juu yaw engine au juu ya kanisa. Inawezekana kwamba alikuwa mashuhuri kwa sababu ya umri, kiasi na uwezo wa kuongeze na asiwe na mamlaka kuliko wengine.

<u>Petro asingekuwa hasa Papa kwanza kwa sababu</u>:

Kristo ndiye kichwa cha kanisa. Akizungumza kuhusu Yesu, Paulo aliandika” “Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote,” Efe. 1:22-23.

Hili limefundishwa pia katika Efe. 5:23 na Kol. 1:18. Maandiko haya yaliandikwa karibu mwaka 64 B.K. Hili lilikuwa muda mrefu baada ya kupaa kwake Yesu karibu mwana 33 B.K. Basi, muda wote huu Yesu alikuwa bado kichwa cha kanisa – na ni kichwa pekee. Hakikuwepo kichwa kinachoonekana duniani. Kwa kuwa Yesu ndiye kichwa cha kanisa, na ni kichwa pekee, tunafikia mwisho kwamba Petro hakuwa kichwa. Wakatoliki wanasema kwamba Yesu ni kichwa cha kanisa mbinguni, lakini wanapigania kwamba Petro alifanywa kichwa kinachoonekana duniani, lakini Yesu hakumfanya mtu yeyote kichwa kinachonekana cha kanisa.

Na tukumbuke kwamba Yesu ana mamlaka Yote mbinguni na duniani, Math. 28:18-20.

II. Kristo ni Msingi wa Kanisa

Ukweli huu uko wazi kabisa:
"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezay kuuweka, isipokuwa ni ule uliokiwhs kuwekwa, yaani, Yesu Kristo," 1 Kor. 3:11.

Kwa hiyo basi, Kristo, sio Petro aliye msingi wa kanisa. Kwa hiyo, wale wafundishao kwamba kanisa lilijengwa juu ya Petro wamo katika kosa. Biblia ni kitabu cha mapatano. Fafanuzi ye yote ya maandiko inaopingana na mengine imepotea.

Natuangalie maandiko mengine ambayo Wakatoliki husema kuwa kanisa limejengwa juu ya Petro:
"Akawaambia, Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simon Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, Heri wewe Simon Bar Yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili; bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuwambia, Wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishi nda," Math. 16:15-18.

Imesemekana kuwa Petro maana yake ni "mwamba" na kwamba Yesu alimwambia atajenga kanisa lake juu yake. Lakini angalia: (1) Petro katika Kiyunani ni Petros, hasa ni jiwe dogo ambalo laweza hata kutupwa (2) Limo katika kundi la kuime (3) Petra, neon lingine la Kiyunani kwamba kama ilivyotumiwa na Yesu maana yake ni eneo kubwa la jiwe, jabali au mwamba (4) Limo katika kundi la kike, na ambalo halina uhusiano na Petro. Jambo hili peke yake linatosha kabisa kusawazisha shauri hili milele. Wakatoliki hubisha kuwa Yesu hakuzungumza katika Kiyunani, na kwamba neon la mwamba katika Aramaic limetumiwa kwa kubdilika-badilika Petros na Petra. Hata hivyo hakuna uthibitisho wa kuwa Mathayo aliandika katika lugha ya Aramaic na hakuna tafsiri za Agano Jiypa katika Aramaic. Mathayo alikuwa Mtume mwenye pumzi ya Mungu, na tunajua kuwa aliandika katika Kiyunan, kama vile tunayo maandiko katika Kiyunani.

<u>Kama kanisa limejengwa juu ya Petro….</u>

a. Lina msingi wa kibinadamu.
b. Limejengwa juu ya mtu aliyemkana Kristo, Math. 26:72.
c. Limejengwa juu ya mtu aliyetukana na kuapa, Math. 26:74.
d. Mathayo 16:18 anapingana na 1 Wakorinto 3:11.
e. Limejengwa juu ya mtu aliyekemewa na Mtume Paulo, Wagalatia 2.
f. Humfanya Petro kuwa mwalimu wa uongo, kwa sababu (1) Petro alisema kuhusu Yesu, "Yeye ndiye jiwe lili lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limekuwa jiwe kuu la pembeni," Mdo. 4:11. (2) Petro anadondoa kutoka Isaya 28:16 kuhusu Yesu, siyo yeye mwenyewe: "Kwa kuwa imeandikwa katika maandiko, Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, na kila amwaminiye hatatahayarika," 1 Pet. 2:6.
g. Limejengwa juu ya mtu aliyeo, Math. 8:14.

III. Ni Hakika Kutokana na Tabia na Maandishi ya Petro kuwa Hakuwa Papa wa Kwanza.

Alijitamblisha nafsi yake kama "Mshiriki wa kazi," 1 Pet. 1:1, na kama "mzee mwezi wao," 1 Pet. 5:1. Hakujiita wala kuruhusu kuitwa "Reverend, Baba au Papa.

Alikataa kusujudiwa nyumbani kwa Korneli, Mdo. 10.

Alisema, "Mimi sina fedha wala dhahabu," Mdo. 3. Papa anaishi katika vyumba vyenye madoido yanavyojulikana siku hizi.

Petro anamwenua Kristo kama Mchungaji Mkuu, 1 Pet. 2:25. Papa anajidai kuwa Mchungaji mkuu yeye mwenyewe.

Petro hakudi kuwa na nguvu za kusamehe dhambi. Katika Mdo. 8, baada ya Simoni kutenda dhambi, Petro alimwambia kutubu na kumwomba Mungu.

Petro hakumteua ye yote kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Yuda, Mdo. 1.

IV. Tabi na Mwenendo wa Mitume Wengine Wahakikish Kwamba Petro Hakuwa Papa.

a. Paulo alimkemea sura kwa sura kwa kufanya unafiki, Wagal. 2:11-14. Wengine walimkemea Petro kwa kula na wa mataifa, Mdo. 11:3.
b. Hawakumwendea Petro kusawazisha maswali.
c. Yakobo na Yohana walimwuliza Kristo kuwapa nafai mashughuli katika Ufalme, Mk. 10:35-40. Kwa nini wafanye hivyo kama Kristo aliisha mfanya Petro kuwa kichwa cha kanisa?
d. Mitume wengine hawakumtazamia Petro kama Paa au mmoja aliye na nguvu au mamlaka kuliko waliyokuwa nayo.
e. Paulo aliliandikia kanisa kule Rumi na aliwataja wengi kwa majina katika waraka kwa Warumi – LAKINI HAKUMTAJA PETRO. Si jambo geni hili! Kama Petro alikuwa Papa?
f. Isitoshe, Paulo aliandika nyarak zinazofahamika kutoka Rumi na hakutaja aina yao yote ya Papa.

V. Kanisa la Kwanza Halikumtambua Petro Kama Papa.

a. Hawakumtambua kuwa na mamlaka zaidi kuliko Mitume wengine. Kama Petro alikuwa Papa, kwanini kanisa la kwanza halikumwendea kusawazisha swala la tohara? (Mdo. 15). Alikuwa ni Yakobo ambaye alisimama na kutoa shauri la mwiso, Mdo. 15:13-22. Kanisa kule Korintho lilipofikiwa na maswali kuhusu ndoa na kula nyama zilizotolewa sadak kwa miungu, hawakumwuliza Petro, bali Paulo (1 Wakor. Sura 7 na 8).
b. Kanisa la kwanza halikumwita Petro kwa vyeo vya heshima, na ukuu. "Hakuitwa Papa, Reverend, Right Reverend, au Baba." Yesu alisema "Wala

msimwite mtu baba duniani maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maan kiongozi wenu ni mmoja naye ndiye Kristo, Math. 23:9-10.

c. Kanisa la kwanza halikumbeba Petro katika kiti kikubwa juu ya mabega, kumsujudia, au kumpa heshima.

VI. Mitume Wote Sawa Katika Mamlaka.

a. Yesu aliwaahidi mitume kuwa watakaa katika viti kumi na mbili vya enzi. "Amini nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na mbili mkiwahukumu makabila kumi na mbili ya Israeli," Math. 28:19.
   Yesu sasa yumo katika kiti cha utukufu (Lk. 24:26; 1 Pet. 1:11; Waebr. 1:3). Muda wa "kuzaliwa kwa pili" ni kipindi hiki cha sasa au labda ingekuwa vigumu kwa mtu kuzaliwa mara ya pili sasa. Tit. 3:5. Mitume walikalia viti vyao vya enzi vya mamlaka siku ya Pentekosti walipopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kuwaongoza katika kweli yote. (Yoh. 16:13; Mdo. 1:5; 2:4); na kuwapa nguvu za ishara kuwawezesha kuliimarisha, kulithibitisha neon lao, Mk. 16:20.
b. Wote walijazwa na Roho Mtakatifu – Sio Petro peke yake, Mdo. 2:4.
c. Petro alisimama pamoja na wale kumi na mmoja, Mdo. 2:14.
d. Mitume wote waliulizwa "tutendeje?" Mdo. 2:37.
e. Wote walipewa neno sio Petro tu, Yoh. 17:14.
f. Wote walipewa neon la upatanisho, 2 Wakor. 5:20.

Maneno yeye pumzi ya Mungu ya Mitume sasa yanakuwa kielelezo katika mambo ya dini. Walipokea neno lao kwa kuvuviwa na Roho Mtaktifu, 1 Wokor. 2:10-13; 2 Pet. 1:21. Wale wanaotembea kinyume cha fundisho waangaliwe na kukataliwa, Rum. 16:17. Wanaokataa kuwasikiliza Mitume sio wa Mungu, 1 Yoh. 4:6.

Maana yake, watu wanahukumiwa katika maisha haya kwa neno lenye pumzi ya Mungu; na lilo hilo tutakutana nalo siku ya hukumu, Yoh. 12:48; Ufu. 20:12.

"Kiti cha enzi" sio kiti cha mbao, bali mahali pa mamlaka. Mitume hawajaj iuzulu. Bado wangali katika viti vyao vya mamlaka. Petro hakuwa na mamlaka zaidi yaw engine kumi na mmoja. Wala hajajiuzulu na kumpa mtu mwingine nafasi yake – wala sio kwa Papa wa Rumi.

Kwa hiyo, kama Mitume wote walilingana katika mamlaka, na kwamba Petro bado anashikilia kiti chake cha enzi, kama Mitume wengine, yamalizia na kufanya isiwezekane kwa Petro kuwa Papa wa kwanza, au kwa Papa wa sasa kuwa mrithi wake.

VII. Mtume Mmoja Hakuweza Kutumia Mamlaka Yake Juu Ya Wengine.

Yesu alifundisha wazi kabisa kwamba kati ya Mitume mmoja asitumie mamlaka yake juu ya wenzie.

"Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu yeyote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu yeyote anayetake kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu," Math. 20:25-27.

Kama Petro alikuwa Papa wa kwanza, ingekuwa ni uvunjaji wa maandiko haya na mamlaka hii.

VIII. Wakatoliki Wanadai Angemweka Mtu Asiyevuviwa Juu ya Mtume Aliyevuviwa.

Inakubaliwa na wengi kwamba Yohana ndiye Mtume aliyekufa mwisho. Baada ya kifo cha Petro, kama mmoja alichukuwa nafasi yake, wasemavyo Wakatoliki – ingawa hawajakubaliana alikuwa nani, alivuviwa kama alivyokuwa Petro, angelikuwa na nguvu za ishara pamoja na kufufua wafu. Kama hakuvuviwa (na hakuwa kama maandiko yatakavyothibitisha) ingekuwa ni kumweka mtu asiyevuviwa kita-katifu.

Kama ni kwa cheo, au mamlaka, Mitume walikuwa wa kwanza. Hakuna hata mmoja bali Kristo na Mungu wangekuwa juu yao. Dai la Wakatoliki ni kinyume cha neon la Mungu kwani tunasoma: "Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa wa kwanza Mitume, wa pili manabii, wa tatu walimu…," 1 Wokor. 12:28.

IX. Aina ya Nafasi Aliyoijaza Petro Haina Nafasi ya Mrithi.

Hasa sehemu hii wengi wameidharau – sio Wakatoliki peke yao na makundi mengine ya dini wanaodai kuwa Mitume wako hai leo.

Neno "Mitume" maana yake ni "aliyetumwa." Yesu alikuwa "Mtume na kuhani Mkuu wa ungamo letu," waebr. 2:1. Alitumwa kutoka mbinguni na Baba yake. Watu waliotumwa na vikundi vya kanisa mara nyingi walifahamika kama "wajumbu (Kiyunani: Mitume) wa makanisa," 2 Wakor. 8:23.

Hata hivyo, Yesu aliwaita, kuwafundisha na kutuma kikundi cha watu kama wajumbe, wasimamizi maalum, washuhuda wa macho. Petro alikuwa mmoja wa watu hawa waliojaza nafasi hiyo na hakuna hata mmoja anayeweza kuwa mrithi wa nafasi hiyo.

## VIFAA VYA UTUME

Watu hawa walipewa mamlaka na nguvu ya kufuna na kufungua, kudhihirisha madhumuni ya wokovu wa mwanadamu. Bwana alivifanya vifaa vya kuwa mtume view na mpaka, na ambavyo vya aina yake kwamba mtu hawezi kuthubutu kuirithi nafasi na kutumia mamlaka yaliyomo bila kujiona kuwa ni mdanganyifu.

Hakuna mtu anayeishi leo anayeweza kukutana na vifaa hivyo. Viko hapa:

1. Alitakiwa awe mshahidi aliyemwona Yesu (a) Hili lilidhihirishwa wakati wa kumteua mmoja wa kuchukua nafasi ya Yuda, Mdo. 1:21-22. (b) Katika nyumba ya Korneli Petro alisema:

"Huyo, Mungu almfufua siku ya tatu, akamjalia kudhihirika, si kwa watu wote, bai kwa mashahidi waliokuwa wamekwisha kuchaguliwa na Mungu, ndio sisi, tuliokula na kunywa naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu," Mdo. 10:40-41. 9c) Paulo alikuwa Mtume maalum, aliyeitwa katika muda unaofaa, 1 Kor. 15:8. Kristo alimtokea Paulo ili awe mshahidi aliyeona ili aweze kufaa kama Mtume, Mdo. 22:14. Kwa kushikilia utume wake Paulo alisema, "Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu?" 1 Kor. 9:1.

2. Mtume alitakiwa kuwa na nguvu za ishara kama vile kusema katika lugha, lugha ambayo hajajifunza, Mdo. 2:4, 6. Uwezo wa kunywa sumu, kuumwa na nyoka asidhuriwe, na nguvu ya kufufua wafu, Mk. 16:17-18; Mdo. 9:40; 20:9, 10) ishara hizi ziliwawezesha Mitume kuimarisha, kuthibitisha, kulikamilisha neon walilolihubiri, Mk. 16:19, 20; Ebr. 2:3-4.

Ishara za Mitume zilifahamika katika karne ya kwanza.

"Kweli ishara za Mitume zilitendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara na maajabu, na miujiza," 2 Wakor. 12:12.

Kuhubiri kwa Paulo kulikuwa "kwa dalili za Roho na nguvu," 1 Kor. 2:4.

Nguvu za ishara zilipatikana kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuwekewa mikono ya Mtume katika siku za kwanza za kanisa.

3. Mtume alitakiwa kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yesu aliwaambia mitume kwamba wataongozwa katika kweli yote na Roho, Yoh. 16:13. Aliwaamuru kungoja Yerusalemu baada ya kupaa kwake na "baada ya siku si nyingi," Mdo. 1:5. Ilikuwa wawe mashahidi wake na kupokea nguvu za kufunga na kufungua, bali ilikuwa lazima wapokee nguvu watakazopew kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu kable hawajaanza, Math. 16:19; Lk. 24:48-49; Yoh. 20:21-23.

Yesu aliwaambia Mitume wake, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yeu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote na Samaria, na hata mwisho wa nchi," Mdo. 1:8.

Hili lilitimia kama siku kumi baadae, Mdo. 2:4. Nguvu za ishara kila siku zikifuatana na ubatizo wa Roho Mtakatifu (tazama pia, Mdo. 10:44, 45).

Siku hizi kuna ubatizo mmoja tu (Waef. 4:5) na ubatizo huu ni katika maji, 1 Pet. 3:20-21. Watu hawawezi kuutumia ubatizo wa Roho Mtakatifu; kwa hiyo ubatizo wa Huduma Kuu, Math. 28:18-20; Mk. 16:15-16, lazima uwe wa maji. Leo hii hakuna ubatizo wa

Roho Mtakatifu na hakuna Mitume ambao bado wako hai. Kwa hiyo, hakuna njia za kupatia nguvu za ishara siku hizi. Hao watoao dai hilo ni waongo.

4. Mtume aliweza kuwapa wengine nguvu za ishara, Mdo. 8:17, 18; 19:6.

Papa sio mshahidi aliyemwona kwa macho yake Yesu. Hana nguvu za ishara. Hajabatizwa katika Roho Mtakatifu. Hawezi kuwapa wengine nguvu za ishara. Kwa hiyo, kama vile Papa hana vifaa alivyokuwa navyo Petro, hana haki ya kujaribu kujiwekea yeye mwenyewe mamlaka aliyokuwa nayo Petro.

**Mamlaka Imekingwa na Vifaa**

Hakuna mtu anayeishi leo aliye na hati ya kusadikisha dai kuwa anajaza nafasi kama aliyokuwa nayo Petro, au labda kwamba anayo mamlaka kama hiyo. Waliojaribu kufanya dai kama hilo katika karne ya kwanza walidhihirishwa na kukemewa:

"Maana watu kama hao ni mitume wa uongo; watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu. Maana shetani mwenyewe ujigeuza awe malaika we nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawa sawa na kazi zao," 2 Kor. 11:13-15.

Wakatoliki hawadai kwamba Papa ni mtume, bali wanadai kwamba ana mamlaka zaidi ile ya Petro aliyekua Mtume. Papa anadai kua ana mamlaka ya kutengeneza na kutunga sheria mpya za dini, kusamehe dhambi, lakini hakuna mtu anayeishi leo aliye na haki ya kudai mamlaka na nguvu kama hizi. Hata Petro hakuwarushusu watu wamsujudie, wala hakudai kuwa ana nguvu za kusamehe dhambi – bali, pamoja na mitume wenginue walidhihirisha kwa Roho njia za msamaha, na njia bora ya kumwabudu Mungu na kumtumikia.

Mtu yeyote anayejdai kuwa Mtume, au kuchukua nafasi hii na kujizoeza katika nguvu za Mitume na ajaribiwe na kuonekana ni mwongo. Haitachukuwa muda kuona kwamba mmoja hana hivyo vifaa vine vilivyoonyeshwa hapa juu. Kanisa la kwanza liliwashihirisha mitume waongo, na Yesu alilisifia Kanisa la Efeso kama ifuatavyo:

"Najua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo," Ufu. 2:2.

Mungu hakuwamuru cheo cha Upapa – watu wamejibunia na kujichukulia mamlaka wanayodai kuwa wanao.

Kwa hiyo, pamoja na mafikara haya uthibitisho ni wa kuelemeza mno kwamba Petro asingekuwa hata kidogo Papa wa kwanza, na kwamba dai la Wakatoliki ni UONGO MTUPU.